Sbimwa

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA KAWAIDA ROBO YA PILI (OKTOBA- DESEMBA) 2023/2024 ULIOFANYIKA TAREHE 05/04/2024 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. **Mh. Leo M. Rushahu** | **-Diwani Nyanza** | **- Mwenyekiti** |
| 2. Mh. Mihayo M. Lutambi | -Diwani Nemba | -Mjumbe |
| 3. Mh. Antidius R. Bruno | -Diwani Nyamahanga | -Mjumbe |
| 4. Mh. Hafsa Galiatano | -Diwani viti maalum | -Mjumbe |
| 5. Mh. Erick R. Method | -Diwani Kalenge | -Mjumbe |
| 6. Mh. Athanas K. Sumbuso | -Diwani Ruziba | -Mjumbe |
| 7. Mh. Asia Nuru | -Diwani viti maalum | -Mjumbe |
| 8. Mh. Ernest M.Kudema | -Diwani Katahoka | -Mjumbe |
| 9. Mh. Mathias J. Lusangija | -Diwani Nyabusozi | -Mjumbe |
| 10. Mh. Mathias F. Nongejiwa | -Diwani Nyamigogo | -Mjumbe |
| 11. Mh. Frolentina Matiba | -Diwani viti maalum | -Mjumbe |
| 12. Mh. Beatrice Oganga | -Diwani viti maalum | -Mjumbe |
| 13. Mh. Amos J. Madebwa | -Diwani Lusahunga | -Mjumbe |
| 14. Mh. Philibert R. Rubula | -Diwani Kabindi | -Mjumbe |
| 15. Mh. Zuhura H. Mmango | -Diwani viti maalum | -Mjumbe |
| 16. Mh.Festo Mtatembwa | -Diwani Bisibo | -Mjumbe |
| 17. Mh. Aniceth Bruno | -Diwani Runazi | -Mjumbe |
| 18. Mh. Apolinary G. Mugarula | -Diwani Nyakahura | -Mjumbe |
| 19. Mh. Petro B. Kizuluja | -Diwani Nyarubungo | -Mjumbe |
| 20. Mh. Jacob H. Jacob | -Diwani Nyantakara | -Mjumbe |
| 21. Mh. Sospeter M. Lunyilija | -Diwani Kaniha | -Mjumbe |
| 22. Mh. Ziyuni Hussein | -Diwani viti maalum | -Mjumbe |
| 23. Mh. David Mwenenkundwa | -Diwani Biharamulo Mjini | -Mjumbe |
| 24. Ndg. Pastory M. Msabila | - A/Tarafa Nyarubungo | -Mjumbe |
| 25. **Ndg. Innocent M. Mukandala** | **-Mkurugenzi Mtendaji (W)** | **-Katibu** |

**B. WATAALAM:**

1. Ndg. Elice B. Francis -Kaimu Mkuu Divisheni ya Utumishi (W)
2. Ndg. George Geofrey -Mkuu Divisheni ya Miundombinu Mjini na Vijijini (W)
3. Ndg. Erick Lubeya -Mkuu Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W)
4. Ndg. Jasphone I. Mukungu -Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu (W)
5. Ndg. Titus Amour -Kaimu MkuuDivisheni ya Elimu Awali na Msingi (W)
6. Ndg. Benedicto Sese -Kaimu Mkuu Divisheni ya Afya (W)
7. Ndg. Namwamini Charles -Mkuu wa Kitengo cha Utamaduni na Michezo (W)
8. Ndg. Abbas ER -Kaimu Mkuu Divisheni ya Ardhi (W)
9. Ndg. Stivin A. Luteganya -Kaimu Mkuu Divisheni ya Elimu Sekondari (W)
10. Ndg. Advera K. Luzibukya -Kaimu Mkuu Kitengo cha Biashara na Uwekezaji (W)
11. Ndg. Shangwe Kabuye -Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo Biharamulo
12. Ndg. Bruno Ngawagala -Kaimu Mkuu Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (W)
13. Ndg. Zainab K. Ally -Kaimu Mkuu Kitengo cha Sheria (W)
14. Ndg. Wanna Nyangaragoro -Mratibu wa TASAF (W)
15. Ndg. Denis Daniel -Kaimu Mkuu Divisheni ya Maendeleo ya Jamii (W)

**C.WAALIKWA:**

1. Mh. ACP. Advera Bulimba -Mkuu wa Wilaya
2. Mh. Robert Malulu -Mwenyekiti Chama Cha Mapinduzi (W)
3. Ndg. Hassan Nshoye -Kaimu Mdhibitiuborawashule (W)
4. Ndg. Fulko Hyera -Katibu TSC (W)
5. Ndg. Leticia Magesa -Kaimu Meneja TANAPA
6. Ndg. Clement Matagi -Kaimu Meneja TANESCO
7. Ndg. Edmund Barongo -Kaimu Meneja BUWSA
8. Ndg.Sylivester Nkaimukilwa -Katibu wa Mbunge

**D.WANAHABARI:**

1. Ndg. Ilen Butabi -Mwandishi wa Habari-FADECO
2. Ndg. Daniel Limbe -Mwandishi wa Habari-NIPASHE
3. Ndg. Yazid Swaibu -Mwandishi wa Habari-ITV
4. Ndg. Allawi Kaboyo -Mwandishi wa Habari-WASAFI MEDIA
5. Ndg. Daudy Yohana -Mwandishi wa Habari- TBC
6. Ndg. William Mpanju -Mwandishi wa Habari- KWIZERA
7. Ndg. Paschal Mussa -Mwandishi wa Habari-Star TV

**E. SEKRETARIETI:**

1. Ndg. Yusuph Mwenda -Mwandishi wavikao
2. Ndg. Eligius Tegarugaba -Mwandishi wavikao

**F. AGENDA ZILIZOJADILIWA**

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Agenda za Mkutano
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa mkutano uliopita wa tarehe **29/11/2023**
4. Yatokanayo na mkutano wa tarehe **29/11/2023**
5. Taarifa za kamati za kudumu
    - Kamati yaUchumi, Ujenzi na Mazingira
    - Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    - Kamati ya Kudhibiti Ukimwi
    - Kamati ya Maadili
    - Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi
6. Taarifa kutoka taasisi mbalimbali
    - BUWSA
    - TANESCO
    - TANAPA
7. Masuala ya kiutumishi
8. Kufunga mkutano

**MUHTASARI. NA: 12/2023-2024. KUFUNGUA MKUTANO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe kwenye Mkutano kisha, alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Mkutano. Mwenyekiti alieleza kuwa huu ni mwendelezo wa Mkutano wa Baraza la Madiwani ambapo walianza na Mkutano wa kujadili taarifa za Kata. Alieleza kuwa taarifa zitakazowasilishwa zimepitia kwenye vikao mbalimbali vya Kamati. Aliwapongeza wajumbe kwa mapokezi mazuri ya viongozi wa chama Taifa na kueleza kuwa miradi iliyotembelewa na wageni hao ilikuwa mizuri. Aidha, alimpongeza Mkuu wa Wilaya kwa kazi nzuri anayoifanya na ushirikiano anaoutoa kwa Halmashauri na alimuomba aendelee kutoa ushirikiano huo.

Mwenyekiti alifungua Mkutano mnamo saa tano na robo (11:15) asubuhi.

**MUHTASARI. NA: 13/2023-2024.KUTHIBITISHA AGENDA ZA MKUTANO**

Jumla ya agenda nane (08) ziliwasilishwa na kuthibitishwa na wajumbe kuwa agenda halali za kujadiliwa na wajumbe.

**MUHTASARI. NA: 14/2023-2024.KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO ULIOPITA WA TAREHE 29/11/2023**

Muhtasari wa Mkutano wa tarehe **29/11/2023** ulisomwa mbele ya wajumbe na kuthibitishwa kuwa kumbukumbu halali ya Mikutano ya Halmashauri.

**MUHTASARI. NA: 15/2023-2024.YATOKANAYO NA MKUTANO WA TAREHE 29/11/2023**

AZIMIO 1: Afisa Elimu Sekondari afuatilie sababu zinazopelekea utoro wa wanafunzi shuleni.

UTEKELEZAJI: Utekelezaji umefanyika na majibu yaliambatishwa *kiambatisho "A"*.

MAJADILIANO:

Wajumbe walieleza kuwa majibu yamejitosheleza.

AZIMIO 2: Barua ya kumkumbusha Mkurugunzi wa KADERES kutekeleza haraka maagizo ya Bodi ya kahawa Tanzania yaliyomo kwenye barua aliyoandikiwa yenye Kumb Na. BA.51/150/04 iandikwe haraka iwezekanavyo.

UTEKELEZAJI: Barua yenye Kumb. Na. BDC/3/3/VOL.V/57 ya tarehe 01/02/2023 iliandikwa kwa Mkurugenzi wa KADERES ilihusu kumkumbushia kulipa wakulima kabla ya tarehe 30/12/2023. Wakulima wa Kahawa wa AMCOS zinazolima kahawa wamelipwa mapunjo yao kasoro AMCOS ya Rubibi ambayo vitabu vyake vilikuwa TAKUKURU. Aidha, wapo wengine toka AMCOS zilizolipwa hawajalipwa kwa madai kuwa walikuwa ni walanguzi na alisema hawezi kuwalipa.

MAJADILIANO:

HOJA: Ni lini wakulima wa Rubibi AMCOS watalipwa mapunjo yao?.

MAJIBU: AMCOS ya Rubibi kulikuwa na matatizo hivyo wakati wakulima wa AMCOS nyingine wanalipwa mapunjo yao nyaraka za wakulima wa AMCOS hiyo zilikuwa TAKUKURU ndio maana hawakulipwa lakini Ofisi ya Mkurugenzi imeomba TAKUKURU isaidie upatikanaji wa nyaraka za wakulima wanaotakiwa kulipwa na badae waendelee

na uchunguzi wao na pindi watakapotoa nyaraka hizo wakulima hao watalipwa mapunjo yao.

HOJA: KADERES alitumia vigezo gani kubaini kuwa baadhi ya wakulima waliouza kahawa zao AMCOS ni walanguzi?.

MAJIBU: KADERES alipewa taarifa na viongozi wa AMCOS na taarifa hizo ndizo alizozitumia kulipa mapunjo ya wakulima.

USHAURI: KADERES ashauriwe kununua kahawa kwa njia ya mnada ili ununuzi wake uendane na bei ya mnada.

MAELEZO: Kabla ya msimu kuanza Mwongozo huwa unatolewa na Bodi ya Kahawa kwa kuzielekeza AMCOS pamoja na vyama vya ushirika namna kahawa zitakavyonunuliwa.

Mjumbe alitoa taarifa kuwa hata vifungashio walivyouzia kahawa wakulima havikurudishwa kwa wahusika.

MAELEZO: Ufuatiliaji utafanyika kulingana na utaratibu utakaokuwa umewekwa kwenye AMCOS hizo.

Mjumbe alieleza kuwa AMCOS ya Rubibi itakuwa na matatizo kwasababu kipindi walipokuwa wanakagua AMCOS hawakupata ushirikiano kwenye kutoka kwenye AMCOS hiyo.

**AZIMIO: Itafutwe orodha ya wakulima ambao hawakulipwa mapunjo yao ya kahawa kwa sababu ya kuwa wao ni walanguzi wa kahawa.**

AZIMIO 3: IundweTimu ya wataalamu kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha ajali ya gari la kubebea wagonjwa (Ambulance).

UTEKELEZAJI: Halmashauri haiwezi kufanya uchunguzi kwakuwa kuna kesi iko mahakamani inaendelea.

MAJADILIANO:

Mwenyekiti alieleza kuwa majibu yaliyotolewa sio sahihi kwasababu ilitakiwa kuchunguzwa ajali iliyotokea Jijini Mwanza.

Katibu alieleza kuwa ajali ilitokea Misungwi-Mwanza na Jeshi la Polisi lilifanya uchunguzi na kupeleka kesi Mahakamani kwa kubainisha wahusika wa ajali hiyo ambapo Mahakama ilitoa hukumu na katika hukumu hiyo ilionekana Dereva wa roli ndiye aliyesababisha ajali.

Taarifa ilitolewa kuwa wakati ajali inatokea inasemekana dereva wa gari la kubebea wagonjwa alikuwa amemuazima dereva mwingine hivyo, dereva aliyeazimwa ndiye aliyesababisha ajali.

MAELEZO: Kutokana na taarifa ya jeshi la Polisi ilionekana mwenye kosa ni dereva wa lori na dereva wa Halmashauri aliyehojiwa ndiye dereva wa gari hilo.

Taarifa ilitolewa kuwa Dereva huyo ni mlevi hata kabla ya ajali ya Mwanza alikuwa amesababisha ajali nyingine hivyo, achukuliwe hatua za kiutumishi.

Katibu alieleza kuwa kwa tukio la ajali ya Mwanza akichukuliwa hatua na wakati taarifa za uchunguzi zinaonesha kuwa hana kosa itakuwa sio sahihi labda ufanyike uchunguzi kwenye masuala ya unywaji wa pombe.

**AZIMIO: Dereva aliyepata ajali na Gari la kubebea wagonjwa Jijini Mwanza arudishwe Makao Makuu ya Halmashauri kwa ajili ya uangalizi wa kina.**

Baada ya yatokanayo na Mkutano wa tarehe 29/11/2023 kujadiliwa, ziliwasilishwa Hoja zilizotokana na kikao cha Kamati ya Chama – Madiwani kilichofanyika tarehe 03/04/2024 na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

HOJA 1: Mwanasheria wa Wilaya aeleze hatua iliyofikiwa juu ya maendeleo ya kesi iliyoko mahakamani (kuhusu dereva aliyeangusha gari la wagonjwa).

MAJIBU: Kesi iliyokuwa mahakamani ilimuhusu dereva wa lori ambapo katika ajali hiyo makosa yalibainika upande wa dereva wa roli Bw. Ramadhani masapala na hatua zilizochukuliwa na mahakama ni;-

1. Kumfungia leseni kwa muda wa mwezi mmoja
2. Alilipa faini ya Tsh 100,000/= badala ya kifungo cha miezi 6

Lakini pia gari hilo liko linatengenezwa na JUBILEE "Insurance" na likitengamaa litarejeshwa Halmashauri.

MAJADILIANO

Wajumbe walieleza kuwa hoja hii imeishatolewa maamuzi.

HOJA 2: Je, michango ya watendaji wa Kijiji na Kata wanaoelekea kustaafu, Halmashauri huwalipia michango yao ya kijamii.

MAJIBU: Kwa sasa hivi Hazina ndio wanahusika na makato na tangu wameanza kukata fedha hizo hakuna malalamiko ya aina yoyote ambayo yameishajitokeza.

Aidha, kwa kipindi cha miaka ya nyuma ambapo watumishi walikuwa wanapokelea mishahara yao Halmashauri kuna baadhi ya watumishi fedha zao hazikupelekwa PSSF na taarifa ya kutopelekwa kwa michango hiyo iliwasilishwa Halmashauri, ambapo Halmashauri ilichukua jukumu la kuwasilisha fedha hizo PSSF na wao walikiri kuzipokea japo mpaka sasa inaonekana PSSF hawajaziingiza kwenye makato ya wahusika. Hivyo, Halmashauri inaendelea na ufuatiliaji wa kuhakikisha zinaingizwa kwenye makato.

MAJADILIANO

Katibu alieleza kuwa tatizo lilitokea kipindi ambacho Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani ilikuwa inalipa watendaji. Baada ya kubainika kuwa kuna deni PSSF kuna fedha zilitolewa kwenye OC kwa ajili ya kuwalipia Watendaji hao lakini pia kuna Watendaji waliokuwa wamelipiwa fedha nyingi tofauti na walizotakiwa kulipiwa hivyo, walikaa na PSSF na kuliweka sawa.

HOJA 3: Je, ni miche mingapi ya Kahawa iliyogawiwa kwa wakulima na usimamizi wake ukoje ili kuhakikisha miche hiyo inastawi kwa kiwango kikubwa?

MAJIBU: Jumla ya miche ya Kahawa 593,912 iligawiwa kwa wakulima 1,733, kiambatisho “A” kiliambatishwa.

Ili kuhakikisha miche hiyo inasimamiwa vizuri Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inaandaa mikataba ya usimamizi kati yake na Maafisa Ugani ambayo itakamilika ndani ya mwezi Aprili 2024 lakini pia Divisheni imendaa fomu maalum za Ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za kila mwezi kuanzia mwezi April 2024. (Nakala za fomu hizo ziliambatishwa) kiambatisho “B”.

MAJADILIANO

USHAURI: Kiongezwe kipengele cha Saini ya mkulima kwenye fomu maalumu za ufuatiliaji na utoaji taarifa za wakulima wa kahawa kila mwezi.

Wajumbe walieleza kuwa taarifa ya idadi ya wakulima waliopanda miche ya Kahawa kwa Kata ya Nyarubungo na Nyanza sio sahihi.

USHAURI: Taarifa ya wakulima waliopanda miche ya kahawa iandaliwe kwa usahihi lakini pia Maafisa Kilimo wasikae maofisini bali watembelee wakulima na kutoa ushauri wa kilimo bora.

HOJA 4: Je ni changamoto ipi inayosababisha kutokufuatwa kwa Ratiba ya vikao iliyopitishwa na Baraza la Madiwani?

MAJIBU: Changamoto zinazopelekea kutofuatwa kwa ratiba ya vikao vya Halmashauri ni pamoja na;-

1. Upungufu wa rasilimali fedha jambo linalopelekea Halmashauri kushindwa kuendesha shughuli zake zote kwa wakati.
2. Mwingiliano wa vikao, mfano ratiba ya vikao vya robo ya pili ambavyo vilitakiwa kufanyika mwezi Januari 2024 havikufanyika kutokana na uwepo wa vikao vya kujadili bajeti ya 2024/2025.
3. Mwingiliano wa ratiba za maelekezo ya kitaifa mfano, wageni wa kitaifa wanaotembelea Wilaya yetu.

MAJADILIANO

Mjumbe alieleza kuwa ratiba ya vikao ipo kikanuni hivyo inatakiwa kufuatwa.

MAELEZO: Katibu alieleza kuwa majibu ni kama yalivyotolewa hii inasababishwa na kutokuwepo kwa rasilimali fedha, ratiba za kitaifa pamoja na mwingiliano wa vikao.

Mwenyekiti alitoa ufafanuzi kuwa Mwezi Oktoba hadi Disemba makusanyo ya mapato huwa sio mazuri hivyo, hazikupatika fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya Mkutano wa Baraza kwa muda huo na Mwezi Januari, 2024 vimefanyika vikao vya kujadili bajeti ya mwaka 2024/2025 pamoja na ugeni wa kitaifa. Lakini pia wajumbe walikaa na kupitisha azimio la kuwa ili vikao vifanyike ni mpaka iwepo fedha hivyo aliwaomba wajumbe watoe maoni yao kama wanatengua azimio hilo.

Wajumbe walikubaliana kuwa azimio hilo hawalitengui bali jambo la msingi ni kila mjumbe kwenye eneo lake ahakikishe anasimamia ukusanyaji wa mapato kwasababu fedha zikiwepo kila kitu kitatekelezwa kwa wakati.

Mwenyekiti aliwataka wajumbe wafanye usimamizi wa ukusanyaji wa mapato lakini pia aliwaomba wakubaliane na hali itakayokuwa inajitokeza kwasababu kuna baadhi ya mambo yanajitokeza na yana athiri ratiba ya vikao.

HOJA 5: Je, Halmashauri ina mpango gani wa kupeleka magari ya wagonjwa katika vituo vya Afya vya Nyakahura na Nyakanazi.

MAJIBU: Magari yapo ila kuna changamoto ya upungufu wa madereva na Halmashauri inafanya utaratibu wa kuomba kibali cha kuajiri madereva hivyo, kibali kitakapopatikana madereva wataajiriwa na kupelekwa kwenye vituo hivyo.

Mwenyekiti alieleza kuwa zinafanyika jitihada za makusudi za kuhakikisha wanapatikana madereva na kwakuwa vituo vina mapato mazuri vinaweza kuwalipa na endapo vitashindwa basi Halmashauri itawalipa.

Baada ya agenda hii Mwenyekiti alimkaribisha Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ili awasilishe salamu za Serikali pamoja na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi ili awasilishe salamu za Chama.

MHESHIMIWA MKUU WA WILAYA

Alianza kwa kumshukuru Mwenyekiti wa Halmashauri kwa kumpa mwaliko wa kuhudhuria Mkutano wa Baraza la Madiwani, alimpongeza kwa namna anavyofanya kazi kwa busara na hekima kubwa na aliwapongeza Waheshimiwa Madiwani kwa namna wanavyofanya kazi na kutatua kero za wananchi kwa wakati pamoja na wanavyoisemea vizuri kazi anayoifanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha anawahudumia wananchi. Alieleza kuwa kiusalama Wilaya iko vizuri kwasababu hakuna matukio makubwa ya kuathiri jamii na pale yanapotokea matukio madogomadogo vyombo vya ulinzi na usalama huwa vinayafanyia kazi na alisisitiza mambo yafuatayo:-

- Miradi viporo ikamilishwe kwa wakati.
- Halmashauri iangalie namna ya kujenga stendi ya kisasa yenye hadhi sawa na Wilaya ya Biharamulo kwa kuzishirikisha hata taasisi mbalimbali za kifedha.
- Iangaliwe namna ya kupata eneo la kujenga maegesho ya magari makubwa Biharamulo Mjini ikiwa ni lengo la kuongeza mapato.
- Halmashauri ihamasishe kilimo cha mazao ya kimkakati ya Kahawa na pamba.
- Wataalamu watumie utaalamu wao vizuri katika kufafanua mambo ambayo yako wazi kwa ajili ya kuwashauri Waheshimiwa Madiwani.
- Usafi wa mazingira usimamiwe kwasababu hali ya usafi hairidhishi kwenye Kata zote.
- Kadri mapato yatakavyopatikana Baraza liangalie namna ya kuweka vitega uchumi katika maeneo ya Hifadhi ya Burigi-Chato ili kuwavutia watalii na Halmashauri kuongeza mapato.

- Waheshimwa Madiwani wakemee na kuhakikisha changamoto ya ucheleweshwaji wa malipo ya mafundi inaisha.
- Inapobainika kuna mgeni ameingia Wilayani ambaye vyombo vya dola vinamtilia mashaka waviachie vifanye kazi pasipo kuviingilia.
- Kila Kata iangalie namna ya kutunza mazingira vizuri kwa kupanda miti pamoja na kutenga maeneo ya kupanda miti kwenye taasisi zinazojengwa.
- Kila mtu kwa nafasi yake ahakikishe anasimamia ukusanyaji wa mapato kwa bidii kwasababu Serikali inategemea mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

MHESHIMIWA MWENYEKITI CHAMA CHA MAPINDUZI

Alianza kwa kuwashukuru wajumbe na kuwapongeza kwa namna wanavyowapigania wananchi na kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwenye maeneo yao. Alimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwa hotuba nzuri na yenye ujumbe mzito aliyoitoa kwa wajumbe na aliwaomba waifanyie kazi kisha, alisistiza mambo yafuatayo:-

- Uwepo ushirikiano baina ya Waheshimiwa Madiwani na Wataalamu.
- BUWSA waboreshe miundombinu ya maji ili wananchi wapate maji ya kutosha kwasababu miundombinu iliyopo imechoka.
- Uongezwe usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- Waheshimiwa Madiwani wafanye mikutano hadi kwenye vitongoji.

NENO LA SHUKRANI (MAKAMU MWENYEKITI)

Alimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwa Salamu za Serikali alizozitoa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na aliahidi kuwa yote waliyoyaongea kwao ni maelekezo hivyo, watayafanyia kazi pia alimuomba Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aendelee kuisimamia Halmashauri katika kila jambo.

**MUHTASARI. NA:16/2023-2024.TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI**

**TAARIFA YA KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA**

Tangu Baraza la Madiwani lifanyike tarehe 29/11/2023 Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira imekaa kikao chake tarehe **18/03/2024**.

Kamati iliazimia, ilishauri, iliomba, ilishukuru na kupitisha mambo yafuatayo:-

A. MAAZIMIO

1. Kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya umiliki wa eneo la ujenzi wa maegesho ya magari makubwa Nyamahanga.
2. Ufanyike ufuatiliaji STAMIGOLD wa kutengeneza barabara ya kuzunguka eneo la maegesho ya magari makubwa Nyakanazi.
3. Utolewe mwongozo ngazi za chini unaotoa maelekezo ya utozaji wa ushuru wa mkaa.

B. USHAURI

i. Itolewe elimu kwa walengwa wa TASAF ili fedha zao wawe wanazitolea benki kwasababu kuna baadhi ya mawakala sio waaminifu wanawapa fedha ambazo ni pungufu na wanazostahili kupata.

ii. Mwaka ujao Halmashauri ijipange ili changamoto ya kununua kahawa za wakulima kwa bei ndogo tofauti na bei ya mnada isijirudie tena.

iii. Chanjo ya mifugo itolewe kwa Wilaya Nzima na kwa aina zote za mifugo.

iv. Maafisa Kilimo walioko ngazi ya Vijiji wasisitizwe kuhudhuria mikutano ya Vijiji na kutoa elimu ya mbolea ya Ruzuku lakini pia wawashauri wakulima aina ya mbolea wanayotakiwa kuitumia kulingana na maeneo yao.

C. MAOMBI

- Wakusanya mapato wa Halmashauri waangaliwe kwasababu kuna baadhi yao hawafanyi kazi ya kukusanya mapato ipasavyo.
- Itolewe elimu ya Kuthibiti UKIMWI katika stendi ya Kikomakoma Kata ya Kabindi na ikiwezekana liwekwe kasha la Kondomu.

D. SHUKRANI

- Kwa Halmashauri kwa kufunga mita na kuwasha umeme kwenye vibanda vya soko la Kabindi.

**Aidha, Kamati ilipokea na kupitisha;**

✓ Taarifa ya mapokezi ya kiasi cha Tsh 2,862,813,250.38 na matumizi ya kiasi cha Tshs 2,637,179,511.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na program mbalimbali iliyotekelezwa kwa kipindi cha Oktoba-Desemba 2023/2024

## TAARIFA YA KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI

Tangu Baraza la Madiwani lifanyike tarehe 29/11/2023 Kamati ya Elimu, Afya na Maji imekaa kikao chake tarehe **18/03/2024**.

Kamati iliazimia, ilishauri, iliomba, ilipongeza na kupitisha mambo yafuatayo:-

A. MAAZIMIO

1. Taarifa ijayo ya lishe ioneshe idadi ya watoto wanaopata na ambao hawapati uji/chakula kwa kila shule.
2. Nakala ya barua zilizoandikwa kwa waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya ya kuwataka kutoa taarifa ya shughuli za lishe na bajeti ngazi vijiji/Kata wapewe Waheshimiwa Madiwani.
3. Iandikwe barua na kutumwa kwa Waheshimiwa Madiwani ikiainisha shule, majina ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu pamoja na kiasi cha fedha wanachopelekewa kwenye shule zao.
4. Kikao kijacho iwasilishwe taarifa ya miradi ya maendeleo iliyokamilika na inadaiwa.
5. Uandaliwe mpango wa kuwajengea uelewa wa pamoja waheshimiwa Madiwani kuhusu mashine za kuongeza virutubishi kwenye vyakula , wapi zinapatika pamoja na gharama zake ili iwe rahisi kwao kufikisha taarifa kwenye jamii.

B. USHAURI

i. Ufanyike ufuatiliaji wa kufahamu vijiji vyenye sheria ndogo za lishe pamoja na ubandikaji wa taarifa za lishe kwenye mbao za matangazo zinazotolewa na watendaji wa Kata

ii. Menejimenti iangalie namna ya kutatua changamoto ya upungufu wa madereva wa magari ya Halmashauri.

iii. Iangaliwe namna ya kupandisha mapato ya iCHF katika Vituo vya kutolea huduma za Afya.

iv. Ufanyike uhamasishaji kwenye jamii wa upatikanaji wa damu salama.

v. Wataalamu wanatakiwa kujipanga kukabiliana na ugonjwa wa Maralia kwenye maeneo ambayo maambukizi yanaonekana kuwa makubwa.

C. MAOMBI

- Maboma ya vyumba vya madarasa yaliyopo Kata ya Lusahunga yawekwe kwenye mpango wa ukamilishaji.
- Wapelekwe walimu kwenye shule zenye upungufu wa walimu Kata ya Kalenge pamoja na mwalimu wa Jiografia na Literature kwenye shule ya Sekondari Munzani.

D. PONGEZI

- Kwa Menejimenti kwa shughuli nzuri za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilizofanyika katika kipindi cha Oktoba-Desemba mwaka wa fedha 2023/2024.

**Aidha, Kamati ilipokea na kupitisha;**

- ✓ Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kwa kipindi cha Oktoba Disemba yenye thamani ya Tshs 4,266,012,853.00.

## TAARIFA YA KAMATI YA KUTHIBITI UKIMWI

Tangu Baraza la Madiwani lifanyike tarehe 29/11/2023 Kamati ya Kuthibiti UKIMWI imekaa kikao chake tarehe **13/03/2024.**

**KIKAO CHA TAREHE 13/03/2024 KILIJADILI MASUALA YAFUATAYO:**

Kamati iliazimia, ilishauri na kupitisha mambo yafuatayo:

A. USHAURI

i. Waathirika wa Virus vya UKIMWI waelimishwe kufika vituo vya kutolea huduma ya Afya na kuchukua dawa za ARVs wenyewe.

ii. Itolewe elimu ya kuelimisha waathirika wa VVU ili waendelee kujitokeza na kupima afya zao.

iii. Elimu ya tohara kwa wanaume iendelee kutolewa kwasababu inachangia katika kuzuia maambukizi ya virus vya UKIMWI.

iv. Serikali iangalie namna ya kuziwezesha usafiri Taasisi mbalimbali zinazoshughulika na utoaji wa huduma kwa waathirika wa Virus vya UKIMWI.

B. MAOMBI

- Wajumbe waliomba kufahamu vikundi vya WAVIU vilipo ili wakavitembelee

## TAARIFA YA KAMATI YA MAADILI

Tangu Baraza la Madiwani lifanyike tarehe 29/11/2023 Kamati ya Maadili imekaa kikao chake tarehe **13/03/2024**.

Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

1. Kuwe na utaratibu maalum katika uchukuaji wa chakula yaani viongozi watangulie alafu wajumbe wa kawaida ndipo wafuatie.

2. Ufanyike usafi wa kina kwenye vyoo vya Halmashauri kwasababu hali ya usafi wa vyoo hivyo hairidhishi.

## TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI

Tangu Baraza la Madiwani lifanyike tarehe 29/11/2023 Kamati ya Fedha Mipango na Uongozi imekaa vikao vitatu tarehe **15/12/2023**, tarehe **05/01/2024,** na tarehe **21/03/2024**.

**KIKAO CHA TAREHE15/12/2023, KILIJADILI MASUALA YAFUATAYO:**

Kamati iliazimia, ilishauri na kupitisha mambo yafuatayo:-

A. MAAZIMIO

1. Afisa Utumishi afanye vikao na watendaji kwenye Kata/Vijiji ambapo mikutano ya vijiji haifanyiki ikiwemo na Kata ya Nyarubungo.
2. Kikao kijacho cha kujadili taarifa za Mwezi Novemba, 2023 iwasilishwe taarifa ya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha katika ujenzi wa vyoo Shule ya Msingi Ntumagu "B"

B. USHAURI

i. Vyanzo ambavyo ukusanyaji wa mapato uko chini ya asilimia 50% Menejimenti ijipange katika ukusanyaji wa mapato ya vyanzo hivyo.
ii. Watendaji wazidi kuelimishwa kuhusu mfumo wa FFARS ili iwe rahisi kwao katika kupokea na kutumia fedha.

**Aidha, Kamati ilipokea na kupitisha;**

- ✓ Taarifa ya mapato ya Tshs 3,892,143,525.75 na matumizi ya Tsh 3,618,363,029.45 kwa Mwezi Oktoba, 2023.
- ✓ Taarifa ya marejesho ya mkopo wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiasi cha shilingi **8,304,000.00** kwa mwezi Oktoba, 2023.
- ✓ Taarifa ya maombi ya kufanya uhamisho wa ndani (reallocation within votes) wa fedha zilizopokelewa nje ya bajeti kwa sekta za elimu sekondari, elimu msingi na afya (Tsh. 908, 245,121.51).

**KIKAO CHA TAREHE 05/01/2024, KILIJADILI MASUALA YAFUATAYO:**

Kamati iliazimia, ilishauri, ilipongeza, iliamua na kupitisha mambo yafuatayo:-

A. MAAZIMIO

1. Zifuatiliwe sababu zilizopelekea Shule ya Sekondari Nyakahura mapato yake kuwa chini ya 50%.
2. Ufanyike ufuatiliaji kwa baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya wa kujiridhisha na mapato yanayokusanywa kwenye vituo hivyo.
3. Vikundi vinavyodaiwa mkopo wa Halmashauri vyenye sifa za kupelekwa mahakamani vipelekwe na kikao kijacho upatikane mrejesho wa kesi hiyo.

B. USHAURI

i. Magari madogo ya abiria yote yasajiliwe na kulipa ushuru.

C. PONGEZI

- Kwa Menejimenti kwa ukusanyaji mzuri wa ushuru wa huduma na usajili wa magari madogo ya Abiria.

D. MAAMUZI

❖ Kahawa zilizonunuliwa na KADERES zisisafirishwe bila malipo ya mapunjo ya wakulima kulipwa.

**Aidha, Kamati ilipokea na kupitisha;**

✓ Taarifa ya marejesho ya mkopo wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kiasi cha shilingi **9,248,500.00** kwa mwezi Novemba 2023.

✓ Taarifa ya mapato ya Tshs 3,887,273,050.43 na matumizi ya Tsh 2,405,658,955.93 kwa Mwezi Novemba 2023.

✓ Mapendekezo ya ujenzi wa shule mbili mpya za Sekondari zitakazojengwa na TANRODS Kata ya Nyakahura-Nyungwe na Lusahuga-Kikoma zitakazogharimu jumla ya Tshs 350,000,000 kila moja.

✓ Mabadiliko ya waweka saini wa kundi "A" na "B" benki akaunti ya BIHARAMULO MISCELLANEOUS DEPOSIT, WOMEN YOUTH DISABILITY BIHARAMULO DC, BIHARAMULO DC IMPREST, BIHARAMULO DC OWN SOURCE COLLECTION kwa kumtoa Majubu John Bernard na kuingia Frank Mathew Minja na akaunti ya WOMEN YOUTH DISABILITY BIHARAMULO DC kwa kumtoa Patricia Peter Sao na kuingia George Stanely Mbilinyi.

**KIKAO CHA TAREHE 21/03/2024, KILIJADILI MAMBO YAFUATAYO;-**

Kamati iliazimia, ilishauri, ilipongeza, ilielekeza na kupitisha mambo yafuatayo:-

A. MAAZIMIO

1. Msimamizi wa Kitengo cha mapato abadilishwe pamoja wakusanya mapato wabadilishiwe vituo na kama kuna ambaye hakusanyi mapato vizuri aondolewe.
2. Watendaji waandikiwe barua ya kuwakumbusha ukusanyaji wa mapato ya vijiji.
3. Viongozi wa jukwaa la wanawake Wilaya waandikiwe barua ya kuwataka wafuate utaratibu wa kiserikali katika utendaji kazi wao.
4. Divisheni ya Mipango iandae mpango wa kuanzisha mradi wa kimkakati katika eneo la soko la Kabindi ili kuiwezesha Halmashauri kuongeza mapato.
5. Kikao kijacho itolewe taarifa ya uwekaji wa vigae kwenye chumba cha darasa shule ya Msingi Biharamulo A na Nyabusozi A
6. Vibanda vilivyojengwa kwenye mipaka ya soko la Kabindi viondolewe.
7. Madeni ya Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na madeni ya Watumishi yalipwe.

B. USHAURI

i. Ufuatiliaji uendelee kufanyika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili mapato lindwa yaweze kuongezeka.
ii. Taarifa za makusanyo ya vijiji zinazoingizwa kwenye taarifa ya mapato na matumizi ziwe ni zile zinazosoma kwenye taarifa za kibenki ili kuwa na uhalisia.
iii. Uandaliwe mwongozo ambao utawaongoza Watendaji wakati wanapoandaa nyaraka za malipo wawe wanaandaa nyaraka zilizokamilika.
iv. Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambazo hazijasoma kwenye mfumo zifuatiliwe na pindi zitakaposoma zifanye shughuli zilizokusudiwa.
v. Miradi iliyopo kwenye hatua za awali za manunuzi yafanyike ili miradi hiyo ianze kutekelezwa.
vi. Mheshimiwa Diwani aendelee kuwasiliana na Mkuu wa Wilaya ili fedha za wanawake zilizochukuliwa na Makamu Mwenyekiti Jukwaa la Wanawake Wilaya zirudishwe.

C. PONGEZI

- Kwa timu ya Menejimenti kwa kufikia 50% ya ukusanyaji wa mapato.
- Kwa Menejimenti kwa utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo.

D. MAELEKEZO

- Majibu ya hoja mpya pamoja na hoja za nyuma yaendelee kutafutwa ili hoja zote zifungwe

**Aidha, Kamati ilipokea na kupitisha;**

- ✓ Taarifa ya mapato ya Tshs 4,054,175,267.46 na matumizi ya Tsh 3,202,546,136.81 kwa Mwezi Disemba 2023.
- ✓ Kamati ilipitisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha Oktoba Disemba, 2023 yenye thamani ya Tshs 7,002,306,569.09.
- ✓ Taarifa ya manunuzi kwa kipindi cha Oktoba –Disemba 2023, yenye thamani ya Tshs 71,659,916.
- ✓ Kamati ilipokea na kupitisha taarifa ya kesi kwa kipindi cha Oktoba Desemba 2023/2024.
- ✓ Ombi la kuhamisha kiasi cha Tsh 30,000,000 mapato ya ndani kutoka Bajeti ya Ujenzi wa Kituo cha Afya Bisibo kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo.
- ✓ Maombi ya idhini mpito (retrospective approval) ya kiasi cha Tshs 29,442,528 iliyotumika kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.
- ✓ Kibali cha kuhamisha fedha kiasi cha Tsh 60,583,872.10 za ujenzi wa matundu 20 ya vyoo kupitia program ya SWASH kutoka shule ya msingi Nyamalagala kwenda shule ya msingi Mlimani.
- ✓ Taarifa ya mapendekezo ya maeneo ya ujenzi wa shule mpya za Sekondari ya Migango, Kitwechembogo, ~~Kalebezo~~ Rusabya, Nyabugombe na Mavota.
- ✓ Ombi la kubadili matumizi ya fedha za mapato ya ndani kiasi cha Tsh 2,100,000 kutoka Kijiji cha Chebitoke kwenda Stendi ya Kikomakoma ili kukamilisha ujenzi wa matundu ya vyoo.

Taarifa zilipokelewa.

MAJADILIANO

USHAURI: Yote yaliyoshauriwa kwenye taarifa hizo yafanyiwe kazi.

**MUHTASARI. NA: 17/2023-2024.TAARIFA KUTOKA TAASISI MBALIMBALI**

**TAARIFA KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI BIHARAMULO (BUWSA).**

Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chujio lenye ujazo wa $M^3$ 650 na njia kuu ya kusafirisha maji toka Ruziba hadi Bomani Biharamulo Mjini ambao utagharimu kiasi cha **Tshs. 843,014,816.00** iliwasilishwa kwa mchanganuo ufuatao;-

i. Ununuzi wa pampu Tshs 168,998,261.00
ii. Ujenzi wa chujio na njia kuu ya kusafirisha maji toka Ruziba hadi bomani Tshs 620,016,555.00.
iii. Kazi ya kuunganisha umeme Gharama zake Tshs 47,000,000.00

Jedwali lililoonesha kazi zilizopangwa kutekelezwa liliambatishwa.

Aidha, taarifa ilielezea mafanikio yatakayopatikana baada ya ujenzi wa tenki kukamilika kuwa ni;-

1. Muda wa kutoa huduma utaongezeka kutoka masaa 10 hadi 12.
2. Kiwango cha kuzalisha maji kitaongezeka toka mita za ujazo 1440 kwa siku hadi mita za ujazo 2440.
3. Idadi ya watu watakaokuwa wanapata huduma ya maji itafikia 95% kwa mjini.

Taarifa ilipokelewa

MAJADILIANO

SHUKRANI: Kwa kazi nzuri inayofanywa na BUWSA ya kuhakikisha wanasogeza huduma kwa wananchi.

OMBI: Kata ya Ruziba hususani Kijiji cha Rugondo ambako maji yanayotumika Biharamulo Mjini yanatoka iangaliwe namna ya wananchi wa kijiji hicho kupatiwa maji.

MAELEZO: Kijiji cha Ruziba kimepelekewa laini ya maji pamoja na DP 2, hivyo, watashirikiana na RUWASA ili kuangalia namna ya kuongeza miundombinu ya maji.

OMBI: Kama Kata ya Nyakahura itaendelea kuhudumiwa na BUWSA basi waongeze bajeti kwasababu Kata hiyo ni kubwa na kama suala la bajeti haliko vizuri basi Kata hiyo irudishwe RUWASA ili waboreshe miundombinu ya maji.

MAELEZO: Limechukuliwa kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa changamoto za maji Kijiji cha Rugondo na Nyakahura atakaa na viongozi wa RUWASA na BUWSA ili waangalie namna ya kulifanyia kazi.

- **TAARIFA KUTOKA SHIRIKA LA UMEME TANESCO BIHARAMULO**

Taarifa iliwasilishwa kuwa, Wilaya ya Biharamulo ni miongoni mwa Wilaya ambazo ni wanufaika wa grid ya Taifa ikiwa na kituo cha kupoza umeme Nyakanazi. Hadi kufikia Disemba 2023 TANESCO Wilaya ya Biharamulo ina hudumia jumla ya wateja 16,034. Taarifa ilielezea miradi inayoendelea kutekelezwa ambapo ni mradi wa REA III round 2, ambao unapeleka umeme katika vijiji 28 vya Wilaya ya Biharamulo kwa gharama ya Tshs 5,970,089,741 kutoka Wizara ya Nishati na mkandarasi ameishawasha umeme kwenye vijiji 14 na kufikia Mwezi Aprili, 2024 mkandarasi atakuwa amewasha umeme kwenye vijiji 14 vilivyobaki, mradi wa umeme COVID 19 ambao unatekelezwa kupitia fedha za COVID 19 zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa gharama ya Tshs 4,111,337,164 katika Kituo cha Afya Bisibo, na vyanzo vya maji 9 na mradi huu umekamilika. Mradi wa umeme Vijiji vya Nyakanazi LOT C, Mradi unapeleka umeme katika vijiji saba na vijiji vyote vimeishawashiwa umeme.

Taarifa ilipokelewa

MAJADILIANO

Mwakilishi wa Meneja TANESCO alijibu hoja za wajumbe na kutolea majibu maombi yaliyotokana na Mkutano wa Baraza la Madiwani wa kujadili taarifa za Kata wa tarehe 4/5/2024 kana ifuatavyo;-

Mjumbe alitaka kupata ufafanuzi juu ya fedha zinazochangishwa kwa wananchi kiasi cha Tsh 30,000 ni za kazi gani.

MAJIBU: Fedha zinazolipwa TANESCO ni gharama za mita pamoja na gharama za kuunganishiwa umeme na fedha hizo huwa zinalipwa kupitia namba ya malipo (contol number). Hivyo, wananchi waelimishwe ili wasije wakawa wanatapeliwa.

OMBI: Umeme upelekwe katika shule zilizojengwa Kata ya Kabindi.

MAELEZO: Litawasilishwa kwa Meneja wa TANESCO ili aliwasilishe mkoani na majibu yatakapotolewa wataenda kuangalia shule hizo.

OMBI: Meneja wa TANESCO aharakishe upanuzi wa mradi wa umeme katika vijiji 2, vitongoji 15, Shule ya Sekondari ya Ruziba, Ofisi ya Kata pamoja na shule za msingi Kata ya Ruziba.

MAELEZO: Watafika eneo la Ofisi ya Kata na shule ili kuangalia namna ya kufikisha umeme kwenye taasisi hizo.

OMBI: Upelekwe umeme katika shule ya sekondari mubaba kwani umeme ni hitaji muhimu kwa shule.

MAJIBU: Litafikishwa kwa mkandarasi ili ahakikishe kabla hajakabidhi mradi anaoutekeleza kijijini hapo anafikisha na umeme katika shule hiyo.

OMBI: Upelekwe umeme katika vitongoji vililivyobaki bila kuwa na umeme katika Kata ya Katahoka

MAJIBU: Litafikishwa kwa mkandarasi ili ahakikishe umeme unafika kwenye vitongoji vyote.

OMBI: Upelekwe umeme katika vitongoji vililivyobaki bila kuwa na umeme katika Kata ya Runazi pamoja na uwekaji wa umeme katika mradi wa maji Migango.

MAJIBU: Jambo hili liko kwenye utekelezaji.

OMBI: Upelekwe umeme katika shule ya Msingi Mafukwe.

MAJIBU: Ameishatoa maelekezo kwa wataalamu kufika kwenye shule hiyo na kuiweka kwenye bajeti ijayo.

HOJA: Mkandarasi wa umeme Musenyi hadi Kisuno analipwa lini ili aweze kuwalipa wananchi wanaomdai?.

MAJIBU: Taratibu za kumlipa zinaendelea na pindi atakapolipwa atawalipa.

OMBI: Waheshimiwa Madiwani wawe wanakutanishwa na wakandarasi kabla hawajaanza kufanya kazi kwenye maeneo yao.

HOJA: Ni lini Mkunkwa na Mpago umeme utawashwa?

MAJIBU: Atalifuatilia na kuhakikisha utekelezaji unafanyika.

Mjumbe alitoa taarifa kuwa katika Kata ya Nyamigogo mkandarasi alienda na ramani nyingine tofauti na ramani ya awali matokeo yake wananchi waliokuwa kwenye ramani ya awali na wakafanya maandalizi ya kuwekewa umeme hawamo.

MAJIBU: Watafika na kulifanyia kazi kwa kumtaka mkandarasi azingatie ramani ya awali.

HOJA: Ni lini kijiji cha Nyakayenze kitaingizwa kwenye mfumo wa ulipiaji wa huduma ya umeme.

MAJIBU: Wataangalia namna ya kulitatua na Mjumbe atapewa majibu.

HOJA: Ni lini waliopitiwa na mradi wa umeme Nyakanazi-Runzewe watalipwa fidia zao baada ya kulipwa malipo ya awali?.

MAJIBU: Watafuatilia na kuona sababu zilizopelekea mpaka muda huu hawajalipwa na kuhakikisha wanalipwa.

HOJA: Ni lini mradi wa umeme kijiji cha Rugese utakamilika?

MAJIBU: Mkandarasi yuko kwenye eneo la mradi hivyo utakamilika hivi karibuni.

HOJA: Ni lini umeme utafika kwenye kijiji cha Rukoke, Kasato na kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri?

MAJIBU: Watafika kupima na kufanya upembuzi wa gharama zinazohitajika kufikisha umeme katika maeneo hayo kulingana na bajeti.

OMBI: TANESCO wapeleke nguzo za umeme katika maeneo ya Chaitaka Kitongoji cha Ng'ambo, Nyamililo Kitongoji cha Nyakatuntu na kibamba kitongoji cha Nyarukongogo.

OMBI: Upelekwe umeme Shule ya Sekondari Lusahunga, maeneo ya Midaho pamoja na Edeni.

MAELEZO: Wataangalia namna ya kujazilizia umeme kwenye maeneo hayo.

USHAURI: Msimamizi wa mradi wa umeme Kalenge ashauriwe kulipa fedha za wananchi wanaomdai na ikiwezekana aondolewe kwenye usimamizi wa mradi huo.

- **TAARIFA KUTOKA SHIRIKA LA HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA (TANAPA)**

Mwakilishi wa Meneje kutoka TANAPA alieleza kuwa kutokana na bajeti ya Serikali wanatamani Hifadhi ya Burigi-Chato iwe kama Serengeti na endapo TANAPA itapata fedha wataweza kufungua barabara ya Katerela ili njia hiyo iweze kutumiwa na watalii, kuanzisha lango lingine la Katete pamoja na Nyungwe ikiwa ni njia mojawapo ya kusaidia wageni kuingia hifadhini. Licha ya nia hiyo nzuri ya TANAPA kuna changamoto ya ukosefu wa miundombinu ya kutumiwa na watalii kama vile hoteli za kitalii kwa ajili ya wageni kupata chakula na vinywaji, ukosefu wa magari kwa ajili ya kubeba watalii, kukosekana kwa vivutio vya asili hususani katika maporomoko ya maji Katerela. Hivyo aliwaomba wajumbe wawekeze katika maeneo hayo au wahamasishe wananchi wawekeze jambo litakalopelekea watalii kukaa muda mrefu na kuongeza pato la Halmashauri. Aidha, alieleza kuwa TANAPA inalenga kuisaidia jamii ambapo kwenye bajeti ya mwaka huu imeomba fedha kwa ajili ya utengenezaji wa madawati japo fedha hizo hazijatolewa. Mwisho aliomba hifadhi zilindwe kwa kutofanya ujangili ili wanyama waweze kuwa wengi kwa ajili ya kuvutia watalii, kisha aliwaomba radhi wajumbe kwa kutowasilisha taarifa ya kimaandishi na aliahidi vikao vijavyo atawasilisha taarifa ya kimaandishi.

Taarifa ilipokelewa

MAJADILIANO

OMBI: TANAPA waangalie namna ya kuboresha miundombinu ya barabara ya kuelekea kwenye mapango ya kale yaliyopo kata ya Bisibo.

HOJA: Mtu akitaka kuingia hifadhini ni utaratibu gani anatakiwa aufuate?

MAJIBU: Kwa mtu binafsi anaandika barua kwa Mkurugenzi Mkuu wa Hifadhi na analipia kiasi cha Tshs 5,900.

Mweneykiti alieleza kuwa wananchi wahamasishwe kupeleka watoto wao wakasomee fani za utalii na hoteli ili Hoteli zitakapojengwa wapate ajira lakini pia wahamasishe ujenzi wa hoteli pamoja na huduma ya usafiri.

**MUHTASARI. NA: 18/2023-2024.MASUALA YA KIUTUMISHI**

**MUHTASARI. NA: 19/2023-20234.KUFUNGA MKUTANO**

Katibu alieleza kuwa yote yaliyojadiliwa yatafanyiwa kazi na utekelezaji wake utaonekana kwenye vikao vijavyo kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge Mkutano. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na alisisitiza mambo yafuatayo;-

- Ufanyike uthibiti wa utoro wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.
- Msimu huu zao la Kahawa linunuliwe kwa njia ya mnada.
- Kila mmoja asimamie na kuhakikisha mapato ya Halmashauri yanakusanywa.
- Miradi viporo ikamilishwe na usimamizi wa utekelezaji wa miradi uimarishwe ili itekelezwe kwa ubora.
- Ofisi ya injinia iwezeshwe usafiri ili wataalamu wa Ofisi hiyo wawe wanafika kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi kwa wakati.
- Suala la usafi wa mazingira lisimamiwe vizuri ikiwemo na ujenzi wa vyoo bora kwa wananchi
- Mafundi wa ujenzi na wazbuni wa vifaa walipwe kwa wakati

Mwisho Mwenyekiti aliwatakia waislamu wote Idd njema na alifunga Mkutano mnamo saa kumi na moja na robo (11:15) jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
|---|---|
| Jina. LEO M. RUSHAHU | Jina. INNOCENT M. MUKANDALA |
| Saini. [signature] | Saini. [signature] |

TAREHE. 31/05/2024